**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**WAKALA YA MAABARA YA VETERINARI TANZANIA**

**VVBD -TVLA TANGA**

**ISO/IEC 17025:201**
**ACCREDITED**

# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA KUUZA MALI CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari ya Tanzania kupitia ofisi yake ya VVBD -Tanga itauza kwa njia ya mnada wa hadhara Magari na vifaa mbali mbali chakavu siku ya Alhamisi tarehe 27 Februari, 2025 katika ofisi zake za VVBD –Tanga.

Wananchi wote watakaoshiriki mnada huo wanaombwa kufika siku mbili kabla ya tarehe ya mnada kwa ajili ya kukagua mali hizo yani Jumanne na Jumatano ya tarehe 25/2/2025 na 26/2/2025 katika Ofisi za VVBD-Tanga Barabara ya Korogwe, Mtaa wa Majani mapana saa 4:00 asubuhi hadi saa 9:30 jioni.

## MASHARTI YA MNADA

1. Gari/Kifaa kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo
2. Magari hayalipiwI ushuru na kodi ya ongezekeo la thamani (VAT), hivyo Mnunuzi atatakiwa kulipia ushuru na kodi zingine kabla ya kuchukua.
3. Kwa Mnunuzi wa vifaa vingine atatakiwa kulipia kifaa alichokipata baada tu ya kumtangaza dalali kuwa mshindi, kifaa ambacho hakijalipiwa kitanadiwa upya. Pia Mnunuzi atatakiwa kuchukua kifaa alichonunua papo hapo tu baada ya kulipia.
4. Mnada utaanza saa 4:00 asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 27 Februari,2025 katika ofisi ya TVLA-Tanga.
5. Ruhusa ya kuangalia gari itatolewa siku mbili (02) kabla ya tarehe ya mnada husika.
6. Mnunuzi wa gari atalazimika kulipa papo hapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari na atakamilisha malipo yote ndani ya muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hilo atakosa haki zote za ununuzi wa gari na amana (deposit) iliyolipwa haitarudishwa.
7. Mnunuzi wa gari atatakiwa kuondosha au kuchukua gari ndani ya muda wa siku saba (07) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
8. Mnunuzi atakaye tamka bei ya juu na kushindwa kulipa, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Imetolewa na:
**MENEJA -VVBD**
**11/02/2025**

TVLA, Mtaa wa Majani mapana, Barabara ya Korogwe, S.L.P 1026 Tanga,
Simu +255 272644572/3, Barua pepe: tvla.tanga@tvla.go.tz, Tovuti: www.tvla.go.tz